

**KITUI WEST SUB-COUNTIES KCSE REVISION MOCK
EXAMS 2015**

**KISWAHILI
KARATASI YA 3
MUDA: SAA 102/3
FASIHI
2½**

SCHOOLS NET KENYA
Osiligi House, Opposite KCB, Ground Floor
Off Magadi Road, Ongata Rongai | Tel: 0711 88 22 27
E-mail: infosnkenya@gmail.com | Website: www.schoolsnetkenya.com

SEHEMU YA A: USHAIRI

1. Lazima

Soma shairi kisha ujibu maswali yafuatayo.

Walimwengu nambieni,
Mie nipate fahamu,
Hawamo vijana wetu,
Meingilia yapi mambo,
Hulkazo hawa wana, tewengu zatia waj,
Sampuli ya hivi viumbe,
Lipi jama uelimisha.

Watembea kwa vishindo,
Miri ndimo ardhi tia,
Ole wako kikutana, nao hawa Masultani,
Takupita ja risasi, vikumbo nusura upigwe,
Wanadi maisha ni shoti,
Wapapie kwa haraka.

Viatu vya chuchumia, ati mbingu wafikila,
Magotini vyabisha hodi, waungwana waole,
Vishati vya kuninginia,
Matumboni ja kima,
Waso haya wana haa,
Wana mji wao ati.

Kikutana nao njiani,
Manywele taambani, maashiki wa rasta,
Bobmal waabudu, ndio jagina wao wana,
Ziki lao la kisasa, lashangaza weni waja,
Sautiyo maskio,
Kusikiza ole wako, tajipata umepokewa,

Na hapa jahazi, langu ufukoni lafikile,
Enyi vijana pilika,
Ya kisasa kufuata,
Bila hadhari si haki,
Tuchuje yenye tijara,
Ya izara tupuzile,
Heshima tudumisha, tamaduni tuienzi.

Maswali

- a) Kwa kutoa mifano, eleza mambo anayolalamikia mshairi. (alama 3)
- b) Eleza ukitoa mifano namna utungo huu umezingatia kaida za ushairi kimuundo. (alama 3)
- c) Andika mfano mmoja wa;
- i) Mistari mishata. (alama 2)
- ii) Msitari kifu. (alama 2)
- d) Eleza namna uhuru wa mshairi ulivyodhihirika katika utungo huu. (alama 4)
- e) Andika ubeti wa nne kwa lugha tutumbi. (alama 4)
- f) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumika katika shairi. (alama 2)
- i) Libasi
- ii) Tijara

SEHEMU YA B: TAMTHILIA***Mstahiki Meya – Timothy Arege***

2. “Kaka zetu hao hawajatoa hela za mkopo hivyo sisi hatuwezi kuwapa ahadi ya kuwaongezea watu mshahara.”
- a) Weka dondoo hili mahali pake. (alama 4)
- b) Mazungumzo haya yanachochewa na nini? (alama 2)
- c) Hawa kaka zetu ni nani? (alama 2)
- d) Ni maudhui gani yanayoendelezwa katika dondoo hili. (alama 2)
- e) Eleza sifa na umuhimu wa mzungumzaji. (alama 10)
3. Wanacheneo walikuwa na haki ya kulalamika. Jadili ukweli wa kauli hii. (alama 20)

SEHEMU YA C: RIWAYA***Kidagaa Kimemwozea – Ken Walibora***

4. “Tembo itakuua ndugu yangu. Punguza ulevi bwana. Siku hizi naona aibu kukuita ndugu yangu”
- a) Fafanua muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
- b) Wahusika hawa wawili ni kama shilingi kwa ya pili. Thibitisha. (alama 16)
5. “Hulka ya Mtemi Nasaba Bora imeshenezewa kila aina ya uovu.” Jadili. (alama 20)

SEHEMU YA D: HADITHI FUPI***Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine – Ken Walibora***

6. Jadili vile mwandishi amefanikisha anwani yake katika hadithi ya “Shaka ya mambo”. (alama 20)
7. “Kama chui aliyevizia windo lake na sasa limetokea akajiandaa”
- a) Eleza muktadha wa dondo hili. (alama 4)
- b) Taja na uonyeshe mbinu mbili zilizotumika katika dondoo. (alama 2)
- c) Eleza kwa ufupi vile mhusika huyu alivyojiandaa. (alama 6)
- d) Eleza sifa nne za anayerejelewa na dondoo. (alama 4)
- e) Kwa kurejelea hadithi hii, jadili changamoto zinazokumba jamii ya kike. (alama 4)

SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI

8. a) Eleza maana ya maigizo. (alama 2)
- b) Fafanua sifa zozote tano za maigizo. (alama 10)
- c) Eleza matatizo yoyote manne yanayomkumba mkusanyaji data ya fasihi simulizi. (alama 8)